

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA **HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA** **SHULE YA SEKONDARI MTOPWA S.L.P 125 NEWALA**

KUMB. NA. SS/JI/VOL.II.20... TAREHE/...../20.....

MZAZI /MLEZI WA

YAH: KUCHAGULIWA KWA MWANAO KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MTOPWA KIDATO CHA KWANZA MWAKA

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Mtopwa kwa mwaka wa kwanza wa masomo nampongeza mwanao kwa kuchaguliwa kwake, akumbuke kuwa hii ni bahati kubwa nay a pekee. shule itafunguliwa tarehe..... hivyo mwanao anatakiwa kuripoti shuleni tarehe saa moja kamili asubuhi.

Pamoja na barua hii nimeambatanisha fomu zifuatazo ili uzingatie na kurejeshwa shuleni siku ya kuripoti:-

1. Orodha ya mahitaji ya shule
2. Sheria na kanuni muhimu za shule hii
3. Fomu ya taarifa binafsi. Njoo nayo ikiwa imejazwa huko nyumbani
4. Fomu (yenye vipimo vya afya) njoo nayo ukiwa umepimwa na kujaziwa katika Hospitali ya wilaya.

karibu sana mtopwa sekondari

.....

GABRIEL C. HAULE

MKUU WA SHULE

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA **HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA** **SHULE YA SEKONDARI MTOPWA S.L.P 125 NEWALA**

FOMU NAMBA 2

FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA KUKUBALI SHERIA NA NAFASI YA SHULE ALIYOPEWA

1. TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

- Jina kamili la mwanafunzi
- Tarehe ya kuzaliwa (ambatanisha na cheti cha kuzaliwa)
- Mahali alipozaliwa (mkoa na wilaya)
- Uraia
- Shule uliyomaliza darasa la saba
- Michezo unayoipendelea
- Nafasi yoyote ya uongozi uliyowahi kushika

2. TAARIFA YA MZAZI/MLEZI

- Jina la mzazi/mlezi
- Kazi ya mzazi/mlezi
- Anuani ya mzazi/mlezi
- Namba ya simu ya mzazi/mlezi

3. MWANAFUNZI

Mimi nimesoma na kuyaelewa yote kwa hiyo nakubali kuipokea/sikubali kuipokea nafasi niliyopewa. ninaahidi kufuata sheria na taratibu zote za shule na kujifunza kwa bidii, kuchapa kazi na nitakuwa na tabia nzuri.

tarehe sahihi

4. MZAZI/ MLEZI

nimehakikisha mwanangu amezisoma na kuzielewa sheria za shule na nimemsisitiza katika hilo.

Tarehe..... Jina Sahihi

1. ORODHA YA MAHITAJI YA SHULE

(A) SARE YA SHULE (WAVULANA)

1. Shati nyeupe mbili (2) za mikono mifupi za kitambaa cha pamba au tetron, zenye kuona (transparent) za kubana au pan asana haziruhusiwi hapa shuleni.
2. Suruali mbili za rangi ya kaki maelezo utapewa unapochukua fomu
3. Viatu vya ngozi vyeusi jozi mbili
4. Raba kwa ajili ya michezo jozi mbili
5. Sweta moja rangi ya bluu
6. Jezi rangi nyekundu na bukta ya bluu kwa ajili ya michezo
7. Soksi nyeusi jozi mbili
8. Tai rangi ya kaki
9. Tisheti nyekundu na suruali nyeusi kwa ajili ya kazi (shamba dress)

(B) SARE YA SHULE (WASICHANA)

1. Wasiovaa hijab shati mbili nyeupe za mikono mifupi za kitambaa cha tetron au pamba nguo za kuonyesha (transparent) na kubana haziruhusiwi hapa shuleni. Na wanaovaa hijabu washone nusu kanzu inayovuka kiuno na juba inayovuka kifua.
2. Sketi mbili za rangi ya damu yam zee. Maelezo utapewa unapochukua fomu.
3. Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili
4. Raba za michezo jozi mbili
5. Tisheti nyekundu na sketi ya rangi ya njano au truck suit rangi ya bluu kwa ajili ya michezo
6. Sweta moja mikono mirefu rangi ya bluu
7. Soksi nyeupe jozi mbili
8. Gauni ya zambarau kwa ajili ya kazi (shamba dress)

(C) ZANA ZA KAZI

1. Jembe kubwa (ngwamba) lenye mpini
2. Kalamu ya wino ya kuandikia, penseli, rula, daftari za kutosha masomo 12 na mathematical set na kamusi (dictionary) moja ya kingereza na kiswahili.
3. Rimu ya karatasi moja a4
4. Fyekeo (slesha/kwanja) na panga

(D) UPATIKANAJI WA CHAKULA SHULENI PAMOJA NA MATIBABU

Kila mzazi / mlezi unapaswa ujiandae kwa mwanao kupata chakula shuleni siku zote za masomo pia swala la matibabu ni wajibu wako kwa mwanao hivyo hakikisha mwanao anajiunga na mfuko wa CHF au NHIF

2. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Rais- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi wa uendeshaji elimu. ukiwa nyumbani utatakiwa kuzisoma kwa makini sheria za shule ambazo zitakuwa mwongozo wako siku zote za maisha yako hapa shuleni. baada ya kusoma na kuzielewa utatakiwa kujaza fomu namba 2 kama kiapo cha kuzielewa na kukubali kuishi kwa mujibu wa sheria za shule. fomu hii utatakiwa kuikabidhi kwa mwalimu atakayekupokea.

A. MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

- i. Wizi
- ii. Uasherati, ushoga, ulawiti na kubaka
- iii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
- iv. Uvutaji wa bangi
- v. Makosa ya jinai
- vi. Kupigana/kupiga au kusababisha ugomvi
- vii. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma au kupoteza
- viii. Kudharau bendera ya taifa
- ix. Kugoma, kuchochea na kuongoza vurugu hivyo kuvunja amani na usalama shuleni/jamii inayokuzunguka
- x. Kuoia ama kua na mchumba au kuolewa

- xi. Kukataa adhabu kwa makusudi
- xii. Utoro
- xiii. Kupata mimba au kuharibu mimba
- xiv. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi

B. UNATAKIWA KUZINGATIA MAMBO YA MSINGI YAFUATAYO

- a) Heshima kwa mwalimu, viongozi, wazazi, wafanyakazi na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni lazima
- c) Kuwahi katika kila shughuli ya shule na nyingine utakazopewa
- d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani ya mipaka hiyo wakati wote ukiwa mwanafunzi wa shule hii.
- e) Kutunza usafi wa mwili na mavazi ya shule
- f) Kuvaa sare ya shule wakati wote utakapotakiwa na kuzingatia ratiba ya shule.

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

**PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL
GOVERNMENT**

NEWALA DISTRICT COUNCIL

MTOPWA SECONDARI SCHOOL, P.O BOX 125 NEWALA

FORM NO. 1

To the medical officer

.....

**RE: REQUEST MEDICAL EXAMINATION OF
(TO BE COMPLEFED BY A GOVERNMENT MEDICAL OFFICER)**

Please examine the above named pupil and give us the report regarding his/her suitability for join form 1 in our school.

1. Pupil full name
2. Blood
3. Stool
4. T.B test
5. Syphilis test
6. Urine examination
7. Eye test
8. Chest test
9. Ears test
- 10.Spleen
- 11.Abdomen
- 12.Pregnancy

ANY ADDITIONAL INFORMATION e.g physical defect or impairment
infection family disease etc

.....
.....
.....
I certify that, the above pupil is suitable / unstable for secondary school
students. If unsuitable give reasons

.....
.....
Name of medical officer: signature

Date official stamp